# HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGU

## MUHTASARI WA MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI KWA AJILI YA KUPITIA TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA ROBO YA PILI OKTOBA - DESEMBA 2023/2024 ULIOFANYIKA TAREHE 16/02/2024 KATIKA UKUMBI WA CCM-MAGU

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA: -**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Mpandalume S. Mpandalume | Diwani Kata ya Nyigogo | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Marco J. Kabadi | Diwani kata ya Kisesa | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Destery Kiswaga | Mbunge Jimbo la Magu | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Peter Deogratius | Diwani kata ya Jinjimili | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Stella A. Ndalila | Diwani V/Maalum kata ya Isandula | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Velina E. Makwandi | Diwani kata ya Isandula | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Herbert G. Faustine | Diwani kata ya Kongolo | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Petro L. Matonange | Diwani kata ya Buhumbi | Mjumbe |
| 9. | Mhe.Hilal.E. Nassoro | Diwani kata ya Nyanguge | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Lucas M. Zabron | Diwani kata ya Lubugu | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Lucas K. Bomoa | Diwani Kata ya Kandawe | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Gerald Paul | Diwani Kata ya Ng'haya | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Anna P. Makula | Diwani V/Maalum kata ya Shishani | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Edda Benjamin | Diwani V/Maalum kata ya Kandawe | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Sambo M. Lupondije | Diwani kata ya Itumbili | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Mashaka Mathias | Diwani kata ya Magu Mjini | Mjumbe |
| 17. | Mhe. John N. Ngagaja | Diwani Kata ya Shishani | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Marco Minzi | Diwani Kata ya Bukandwe | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Bunyanya K. John | Diwani kata ya Bujora | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Deleli L. Mazoya | Diwani kata ya Bujashi | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Secilia E. Hima | Diwani V/maalum kata ya Kabila | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Nduhi L. Kabadi | Diwani kata ya Mwamabanza | Mjumbe |
| 23. | Mhe. Faustine Makingi | Diwani kata ya Sukuma | Mjumbe |
| 24. | Mhe. Mary Kaligi | Diwani V/Maalum kata ya Kitongosima | Mjumbe |
| 25. | Mhe. Hilder A. Mdachi | Diwani V/maalum kata ya Kisesa | Mjumbe |
| 26. | Mhe. Butogwa B. Mayala | Diwani V/Maalum kata ya Bujora | Mjumbe |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 27. | Mhe. John M. Mitubo | Diwani kata ya Chabula | Mjumbe |
| 28. | Mhe. Ng'wanabuta Enos | Diwani kata ya Lutale | Mjumbe |
| 29. | Mhe. Diana E. Philimon | Diwani V/ Maalum Kata ya Kitongosima | Mjumbe |
| 30. | Mhe. Gunze Philipo | Diwani kata ya Mwamanga | Mjumbe |
| 31. | Mhe. Gilang'hinda Busiga | Diwani kata ya Nkungulu | Mjumbe |
| 32. | Mhe. Edward J kihamba | Diwani kata ya Kabila | Mjumbe |
| 33. | Mhe. Machibula L. Deus | Diwani kata ya Kahangara | Mjumbe |
| 34. | Mhe. Silas C. Kipeja | Diwani Kata ya Kitongosima | Mjumbe |
| 35. | Mhe. Rebeca J. Kipeja | Diwani V/Maalum Kata ya Kahangara | Mjumbe |

**WAJUMBE WASIOHUDHURIA KWA TAARIFA:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Dr. Stergomena Tax | Mbunge Mteule | Kwa taarifa |
| 2. | Mhe. Mary F. Masanja | Mbunge Viti Maalum | Kwa taarifa |

**WATENDAJI WALIOHUDHURIA:**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bi Fidelica G. Myovella | Mkurugenzi Mtendaji H/W ya Magu |
| 2. | Bw. Henry J. Sadatale | Mkuu wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali watu |
| 3. | Bw. Amandus L. Mboya | Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii |
| 4. | Bw. Peter M. Manoko | Mkuu wa Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi |
| 5. | Bw. Alphonce Awaki | Mkuu wa Sehemu ya Kilimo |
| 6. | Bw. Mohamed Kyande | Mkuu wa Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi |
| 7. | Bw. Mwagala Masunga | Mratibu wa Shughuli za Uchaguzi |
| 8. | Bi. Emmanuela P. Chacha | Kaimu Katibu TSC |
| 9. | Bw. Francisco M. Ndazi | Mkuu wa Kitengo cha usimamizi wa taka na usafi wa mazingira |
| 10. | Bw. Peter M. Mujaya | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Michezo, Utamaduni na Sanaa |
| 11. | Bi. Leticia Nyakahinga | Kaimu Mkaguzi Mkuu na Mdhibiti Ubora wa Shule |
| 12. | Bw. Joseph J. Mtengu | Mkuu wa Kitengo cha Fedha na Uhasibu |
| 13. | Bi. Kuruletera Florence | Mkuu wa kitengo cha Ukaguzi wa ndani. |
| 14. | Adv. Selestina Kunambi | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Sheria |
| 15. | Bi. Glory V. Mtui | Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi |
| 16. | Bw. Paschal Mashamba | Kaimu Mkuu wa Kitengo |

| | |
|---|---|
| | cha Mawasiliano Serikalini. |
| 17. Bi. Beatrice B. Balige | Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari |
| 18. Bw. Wilfred Majigo | Mkuu wa Idara ya Ardhi |
| 19. Bw. Eusebius Chanjali | Kaimu Mkuu wa Idara ya Huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe |
| 20. Bw. Simioni Mwita | Kaimu Afisa Usafirishaji. |
| 21. Bw. Ngussa M. Buyamba | Mkuu wa Kitengo cha Maliasili na Uhifadhi wa Mazingira |
| 22. Bw. Yusuph Digossi | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini. |
| 23. Bi. Martha Godi | Afisa Utumishi |
| 24. Arch. Herieth Mdoe | Kaimu Mkuu wa Idara ya Miundombinu Maendeleo ya Vijiji na Mijini |
| 25. Bw. Fundikira Saidi | Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Magu. |
| 26. Dr. Daniel Sanyenge | Mratibu TASAF |
| 27. Bw. Festus P. Kisanga | Kaimu Mkuu wa Idara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji |

**KAMATI YA ULINZI NA USALAMA:**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bi. Rachel S. Kassanda | Mkuu wa Wilaya Magu |
| 2. | WOI.Thobias K. Charles | Mshauri wa Jeshi la Akiba |
| 3. | Bw. Elias D. Mwandobo | Mkuu wa Usalama (W) |
| 4. | Sp. Kiyelu Y. Bayinga | Mkuu wa Magereza (W) |
| 5. | Bw. Francis Nyerere | Kaimu Kamanda wa TAKUKURU (W) |
| 6. | A/Insp Victor Adam | Afisa Usalama |
| 7. | A/Insp Gastone C. Tigulabwa | Kamanda wa Zimamoto (W) |
| 8. | Sp. Haji F. Makame | Mkuu wa Polisi (W) |
| 9. | Bi. Jubilate W. Lawuo | Katibu Tawala (W) |

**WAGENI WAALIKWA:**

| | |
|---|---|
| 1. Bw. Lubapula Mayombya | Kaimu Meneja RUWASA (W) |
| 2. Bw. Samwel N. Thomas | Kaimu Meneja Mwauwasa (W) |
| 3. Eng. Mussa Mzuba | Meneja TARURA (W) |
| 4. Bw. Samwel C. Temu | Meneja NIDA |
| 5. Bw. Enos N. Kalambo | Mwenyekiti CCM (W) |
| 6. Bw. Antoni Mtewele | Kaimu Meneja TRA |

**MAAFISA TARAFA**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bw. Emmanuel M. Ndillah | Afisa Tarafa Itumbili |
| 2. | Bw. Anthony M. Ntarle | Afisa Tarafa Sanjo |
| 3. | Bi. Grace M. Msilanga | Afisa Tarafa Ndagalu |
| 4. | Bi. Sylyvia L. Mayala | Afisa Tarafa Kahangara |

**WATENDAJI WA KATA**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bw. Evodius Mushema | Mtendaji wa Kata ya Mwamabanza |
| 2. | Bi. Salome Julius | Mtendaji Kata ya Bujora |
| 3. | Bw. Ernest M. Mkama | Mtendaji wa Kata ya Lubugu |
| 4. | Bw. Azimio Gervas | Mtendaji wa Kata ya Kahangara |
| 5. | Bw. Ezekiel W. Segeredi | Mtendaji wa kata ya Kitongosima |
| 6. | Bw. Essau Gwangimeza | Mtendaji wa Kata ya Jinjimili |
| 7. | Bw. Emmanuel C. Saendah | Mtendaji wa Kata ya Mwamanga |
| 8. | Bw. Wilbroad K. Mbuga | Mtendaji wa kata ya Nyanguge |
| 9. | Bi. Eunice S. Sangila | Kaimu Mtendaji wa Kata ya Kongolo |
| 10. | Bw. John C. Mabiti | Mtendaji wa Kata ya Isandula |
| 11. | Bw. Daniel J. Sahani | Mtendaji kata ya Chabula |
| 12. | Bw. Ismail V. Oyuga | Mtendaji wa Kata ya Kisesa |
| 13. | Bw. Philipo J. Lusesa | Mtendaji wa Kata ya Nyigogo |
| 14. | Bw. Michael Brasio | Mtendaji wa kata ya Buhumbi |
| 15. | Bi. Catherine C. Matutu | Mtendaji wa Kata ya Shishani |
| 16. | Bw. Jeremiah A. Kalwani | Mtendaji wa Kata ya Ng’haya |
| 17. | Bw. Juma R. Kashilimu | Mtendaji wa Kata ya Magu Mjini |
| 18. | Bw. Leonard L. Nzabhayanga | Mtendaji wa Kata ya Kabila |
| 19. | Bi. Devotha M. Robert | Mtendaji wa Kata ya Sukuma |
| 20. | Bi. Lina D. Amata | Mtendaji kata ya Itumbili |
| 21. | Bw. Emmanuel C. Sengerema | Mtendaji wa Kata ya Bukandwe |
| 22. | Bw. Ichobe M. Nyasanga | Mtendaji wa kata ya Bujashi |
| 23. | Bw. Charles M. Mabona | Mtendaji wa Kata ya Nkungulu |
| 24. | Bw. Victor M. Kisamu | Mtendaji wa Kata ya Lutale |
| 25. | Bw. Patrick Mkame | Mtendaji Kata ya Kandawe |

**SEKRETARIETI:**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bi. Happiness J. Mbalilaki | Mwandishi wa Vikao |
| 2. | Bi. Judith J. Aron | Mwandishi wa Vikao |
| 3. | Bw. Jordan F. Mchongi | Mwandishi wa Vikao |

**MUHT. NA. 13/2023/2024: - KUFUNGUA KIKAO:**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili aweze kufungua mkutano wa Baraza la Madiwani kwa ajili ya kupitia taarifa za utekelezaji robo ya pili Oktoba – Desemba, 2023/2024.

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe na wageni waalikwa kwenye mkutano na kuwataka wachangie agenda zilizopo mbele yao. Baada ya kusema hayo, Alifungua kikao mnamo saa 4.00 asubuhi.

**MUHT. NA. 15/2023/2024: TAARIFA ZA UTEKELEZAJI KUTOKA KATANI**

Kata zilizowasilisha taarifa za utekelezaji kutoka kata ni kama ifuatavyo; -

Kata ya Bujora, Lubugu, Nyigogo, Lutale, Ng'haya, Mwamabanza, Kitongosima, Jinjimili, Kisesa, Shishani, Itumbili, Kahangara, Nkungulu, Magu mjini, Chabula, Sukuma**,** Mwamanga, Buhumbi, Isandula, Nyanguge, Bujashi, Bukandwe, Kongolo, Kabila, Lutale

**MUHT. NA. 16/2023/2024: MASWALI YA PAPO KWA PAPO**

Hakuna maswali yapo kwa papo yaliyowasilishwa mezani kwa Mwenyekiti.

**MUHT. NA. 18/2023/2024: KUWASILISHA TAARIFA ZA KAMATI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI KWA KIPINDI CHA OKTOBA HADI DESEMBA, 2023/2024**

Wenyeviti wa kamati za kudumu za Halmashauri waliwasilisha taarifa za kamati katika kipindi cha robo ya pili Oktoba hadi Desemba, 2023/2024 ili zijadiliwe na wajumbe kama ifuatavyo: -

- Kamati ya UKIMWI
- Kamati ya Elimu, Afya na Maji
- Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira
- Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa wajumbe walizipokea na kuwa kumbukumbu za Halmashauri.

**MUHT. NA. 19/2023/2024: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA ROBO YA PILI OKTOBA HADI DESEMBA, 2023**

Mkuu wa Idara ya Mipango kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji aliwasilisha taarifa ya utekelezaji katika kipindi cha robo ya pili Oktoba hadi Desemba, 2023. Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuridhia kuwa katika robo ya pili shughuli za utekelezaji wa miradi zimefanyika vizuri na kusisitiza kuwa wataalam waendelee kuzikamilisha kwa wakati na kwa ufanisi.

**MUHT. NA. 20/2023/2024: MASWALI KUTOKA VYAMA VYA SIASA**

**Swali na.01:**
Kwanini Barabara ya Mwanza – Musoma kipande cha Nyanguge – Bulalu kimetengenezwa chini ya kiwango?

**Majibu:**

Barabara hii inasimamiwa na Meneja wa Wakala wa Barabara Mwanza (TANROADS).

Mheshimiwa Diwani Kata ya Ng'haya alishukuru kwa fedha zinazotolewa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan na kusema kuwa TANROADS hawajengi Barabara hizo kwa uimara na viwango vinavyotakiwa lakini pia mitaro inajengwa na hakuna sehemu ya kuvukia. Hivyo alishauri mitaro ijengewe vizuri na sehemu za kuvukia ziwekwe.

Mheshimiwa Diwani kata ya Magu Mjini alisema kuwa swali hili limekuwa likijirudia hivyo TANROADS hawatendi haki katika utekelezaji wa miradi ya Barabara kwa kuwa kabla ya kumalizia mwezi mmoja Barabara hiyo tayari imeanza kuharibika. Pia alisema kuwa Barabara ya kuingia stendi ya Magu Mjini imejaa mashimo hivyo madereva hukwepa kuingia ndani ili magari yasiharibike hii inapelekea Halmashauri tunapoteza mapato.

Mheshimiwa Diwani viti maalum kata ya Shishani alisema kuwa TANROADS walitengeneza Barabara ya Shishani ila hawakuweka Kalavati imara ambapo Kalavati hilo limebomoka, alishauri kuwekwa Kalavati imara katika Barabara hiyo.

Mheshimiwa Diwani kata ya Kongolo alishauri masuala haya ni vyema yakazungumziwa kwenye vikao vya Halmashauri ya Wilaya (DCC) au Halmashauri ya Mkoa (RCC) hivyo aliomba Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi Mtendaji walifanyie kazi kwenye vikao muhimu kama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti alisema kuwa watazungumza masuala hayo kwenye vikao mpaka vya Mkoani ili kero hiyo ipate ufumbuzi. Aliongezea kwa kusema kuwa wana - Magu hawajaridhishwa na ukarabati wa ujenzi uliofanywa na TANROADS.hasa kwa Barabara za Mkoa wa Mwanza.

**Swali na. 02:**

Lini Barabara ya Lumve Sekondari itakamilishwa kwani boma limekamilika tangu mwaka 2017.

**Majibu:**

Halmashauri itaendelea kukamilisha maabara kadri fedha zinavyopatikana, aidha kwa mwaka wa fedha 2024/2025 imetengwa fedha kiasi cha Tshs. 210,000,000/= za ukamilishaji wa maabara kutoka Serikali Kuu shule za sekondari Deleli maabara tatu (03), Kabale maabara mbili (02) na Nyantimba maabara moja (01).

**Swali na.03:**

Kwanini gharama za maji zimepanda kutoka Tshs. 1,300/= hadi 2,000/=

**Majibu:**
Gharama hizi zimepanda kutokana na mpango wa biashara wa miaka mitatu ulioandaliwa na timu ya uendeshaji kwa kuzingatia mwongozo wa kuandaa mpango wa biashara na mwongozo wa ukokotoaji wa bei za maji kwa wateja wa vituo vya maji binafsi na majumbani. Pia kutokana na mapendekezo ya bei yaliyowasilishwa kwa Mkurugenzi Mkuu na kujadiliwa na Menejimenti ya RUWASA na kupelekwa kwenye Bodi ya Wakurugenzi kwa ajili ya kupata idhini hivyo na kuwasilishwa kwa chombo husika kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Diwani kata ya Nyanguge alisema bei ya maji imepanda RUWASA ila MWAUWASA bado wanalipisha bei zile zile za mwanzo. Kabla ya kupandishwa kwa bei walishirikishwa wananchi na walipendekeza Tshs. 1,000/= hivyo kwa bei walizoleta wao ni tofauti na mapendekezo ya wananchi hali hiyo imeleta taharuki kwa wananchi.

Mheshimiwa Diwani kata ya Ng’haya alisema upandishaji wa bei ya maji umefanyika kwa baadhi ya maeneo na mengine yameachwa na bei za zamani jambo ambalo linatafsiriwa kuwa vijijini kuna hela zaidi wakati huko ndiko kuna shida zaidi, hivyo alitaka kujua RUWASA wameruhusiwa kutoza maji kwa bei zipi.

Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Magu alisema kuwa bei ya maji imepandishwa kutoka 1500 hadi 2000 ambapo sio sawa. Aliomba gharama halisi za uendeshaji zijulikane ili wajumbe wajue kama bei hizo zinaendana na gharama za malipo ya huduma ya maji. Aliongeza kwa kusema kuwa awali Wizara ya Maji ilileta utaratibu kuwa kila Mkoa wakae pamoja na kuweka gharama elekezi wakihusishwa wataalam wa mpango biashara ambapo wazingatie na kuangalia vitu vinavyotumika ambavyo ni kama vile dawa, mitambo, umeme, mishahara ya wafanyakazi ili bei zipendekezwe kutokana na teknolojia inayotumika, hivyo Bodi ya RUWASA iliboresha na kuchakata mpaka kufikia bei hizo kwa uhalali wa kisheria.

Mheshimiwa Diwani kata ya Mwamanga alisema kuwa zinapoanzishwa “CPUSO” hupewa mamlaka ya kusimamia mradi na sio kupandisha bei ya maji. Hivyo bei hizo yawezekana zimeombwa kwa barua sio kuwa Wizara husika imetoa bei hizo ambapo imebainika kwenye barua hii iliyoletwa ikiainisha bei za maji mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti alisema kuwa wanatakiwa kukutana na watu wa RUWASA na MWAUWASA tarehe 19.03.2024 katika Ofisi za Mkuu wa Wilaya ili walijadili suala hilo kwa kina na hatimaye bei hizo zijulikane.

**Swali na.4:**

Idara ya Elimu inampango gani kuhakikisha sifuri zinapungua kama si kuisha.

**Majibu:**

Idara imejipanga kutekeleza mpango wa kutokomeza sifuri kama ifuatavyo: -

- Kusimamia ufundishaji na kuchukua hatua kwa walimu watoro
- Kudhibiti utoro wa wanafunzi wanaopelekea kupata sifuri
- Kushirikiana na jamii kutoa chakula cha mchana kwa wanafunzi
- Kuimarisha Uongozi wa Shule.

**Swali na.5:**

Mwatelesha Shule ya Msingi lini itajengewa vyoo vya wanafunzi?

**Majibu:**

Shule ya Msingi Mwatelesha imewekwa kwenye mpango wa “Boost” awamu ya pili kujengewa matundu ya vyoo kumi na tatu (13).

Mheshimiwa Diwani kata ya Kandawe alisema kuwa Shule ya Msingi Mwatelesha ilianzishwa miaka ya zamani sana na kuiomba Halmashauri ya Wilaya ione umuhimu wa kupeleka huduma ya vyoo kuliko kusubiri shule hiyo kufikia hatua ya kufungiwa.

Mwenyekiti alisema kuwa shule zote za msingi na sekondari zifanyiwe ukaguzi na kubaini vyoo vyenye kasoro ili kwa idadi hiyo mapato ya ndani yaweze kutumika katika ujenzi na ukarabati.

**SALAMU KUTOKA MEZA KUU NA MUALIKWA KUTOKA NIDA WILAYA YA MAGU**

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe wa meza kuu na mgeni kutoka Nida kwa ajili ya kuongea na wajumbe wa Kamati.

Meneja wa NIDA tawi la Magu alizungumzia kuhusiana na kero iliyokuwepo siku za nyuma katika usajili na upatikanaji wa vitambulisho kuwa sasa tatizo hilo limetatuliwa. Alisema kuwa Watendaji wa Kata ndio wasambazaji wa vitambulisho kwa wananchi ambapo hurahisisha upatikanaji wa vitambulisho hivyo kwa kila kata wakisaidiana na Ofisi ya NIDA. Aliomba wenyeviti na maafisa tarafa wasaidie katika utoaji elimu juu ya umuhimu wa kujisajili na kisha kupatiwa vitambulisho hivyo. Alimalizia kwa kusema kuwa mpaka sasa vitambulisho elfu sabini vimekwisha tengenezwa katika Wilaya ya Magu na wananchi wengi wao wamekwisha patiwa vitambulisho hivyo na wale wote ambao bado

zoezi la kuvisambaza katika kata husika limefanyika hivyo wafanye jitihada za kuvichukua katika kata zao.

Mheshimiwa Diwani kata ya Magu Mjini aliomba mashine za usajili zipelekwe kwenye kata na tarafa ili wananchi wapatiwe huduma ya vitambulisho kwa urahisi.

Baada ya maoni na ushauri kutoka kwa wajumbe Meneja wa NIDA Wilaya ya Magu alitoa wito kwa watendaji wa kata kukaa na kuona namna gani wananchi watasaidiwa kwa urahisi lakini suala la kutoa huduma kwenye kata alilichukua na kuahidi kuwa litafanyiwa kazi.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) aliwashukuru wajumbe wote kwa michango mizuri waliyoitoa kwenye mkutano. Aliwakumbusha kuwa mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi hivyo waendelee kuombea na kukisemea vizuri Chama Cha Mapinduzi.

Makamu Mwenyekiti alimpongeza Mwenyekiti kwa namna alivyoongoza mkutano na wajumbe kwa michango yao yenye tija. Alisisitiza kuwa watendaji wa Kata walipwe stahiki zao mapema pindi wanapohama. Pia alimshukuru Mhe. Mbunge wa Jimbo la Magu kwa kuendelea kuisemea vyema Wilaya ya Magu pamoja na Mheshimiwa Rais kwa jinsi anavyoendelea kuleta fedha kwa ajili ya miradi ndani ya Wilaya ya Magu.

Mheshimiwa Mbunge Jimbo la Magu aliwapongeza wajumbe wote wa Baraza kwa michango mizuri na kusema kuwa mahitaji katika Wilaya ni mengi hivyo kwa kila fungu tunalopata tujitahidi kuitumia vizuri na miradi iwe ya kuridhisha.

Mkuu wa Wilaya alimpongeza Mwenyekiti kwa namna alivyoongoza mkutano na kusema kuwa mwaka huu kuna uchaguzi wa Serikali za Mitaa hivyo Madiwani na Watendaji wanapofanya vikao katika kata zao wasisitize kuhusu zoezi hilo. Pia alizungumzia suala la wanafunzi kuripoti mashuleni kuwa hatujafikia asilimia inayotakiwa hivyo tushirikiane na Watendaji ili kuhakikisha wanafunzi ambao hawajaripoti mashuleni waweze kuripoti. Aidha alitangaza kuwa tarehe 08/03/2024 ni siku ya wanawake duniani na kutambulisha sare itakayotumika siku hiyo na wanaume wawepo kusherehekea siku ya mwanamke duniani.

**MUHT. NA. 21/2023/2024: MATANGAZO KUTOKA KWA MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI**

Mkurugenzi Mtendaji aliwapongeza wajumbe kwa namna walivyotoa michango yao katika mkutano. Aliwashukuru na kuwapongeza watendaji kwa jinsi wanavyofanya kazi kubwa hasa katika kuhakikisha mapato hayashuki na aliwaelekeza waendelee kusimamia mapato ili kudhibiti mianya yote ya mapato.

Alizungumzia kuhusu stahiki za watendaji kuwa huwa zinapitishwa kwa wakati, aliomba sehemu zenye changamoto wasisite kumuona ili ziweze kutatuliwa kwa wakati.

Chanjo ya Surua inaendelea kutolewa na watoto wanaendelea kufikiwa kwa ajili ya kupatiwa chanjo hiyo. Hivyo alisisitiza wajumbe wazidi kuhakikisha zoezi hilo linaendelea na watoto wapelekwe kwa wingi.

Alisisitiza kuendelea kuwahimiza wazazi kuwapeleka wanafunzi ili waripoti mashuleni. Wakuu wa shule watoe taarifa kuhusu wazazi wanaosumbua na kuwazuia wanafunzi Kwenda shule. Alimshukuru Mbunge na Mwenyekiti kwa kushirikiana katika kutekeleza miradi ya maendeleo na shughuli zote za Halmashauri ya Wilaya.

**MUHT. NA. 22/2023/2024: KUFUNGA MKUTANO**

Katibu wa mkutano alimkaribisha Mwenyekiti ili afunge mkutano, Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa kuhudhuria na kwa jinsi walivyotoa michango yao yenye tija kwa ajili ya maendeleo ya Halmashauri.

Alizungumzia kuhusu bajeti tuliyonayo tuendelee nayo vizuri japo baadhi ya maeneo kama ardhi imetuweka katika hali mbaya kimapato. Alimuomba Mkuu wa Wilaya aendelee kutoa ushirikiano katika zoezi la upimaji wa viwanja. Aliwaomba viongozi waendelee kusimamia miradi pia alielekeza Mkaguzi wa Ndani awakabidhi Mkuu wa Wilaya pamoja na Kamati ya Ulinzi na Usalama nyaraka za ujenzi wa maabara ya Masengese ili maamuzi ya mradi huo yaweze kutolewa.

Alimpongeza Mtendaji wa Kata ya Bukandwe kwa kusimamia mapato vizuri na kuwahimiza watendaji wote wajitahidi kusimamia na kuhakikisha mapato yanayokusanywa yanaendana na uhalisia ili kuweza kufikia malengo ya bajeti. Baada ya maneno hayo alifunga mkutano mnamo saa 8:30 mchana.

**MUHTASARI UMETHIBITISHWA**

_____________________________ _____________________________

**KATIBU** **MWENYEKITI**

**TAREHE** _______________________